



NI MWEZI WA MARIA

NOVENA YA BIBI YETU WA FATIMA

TAREHE 04-12/MAY

SALA YA MWANZO:

1.Sala ya Mwanzo Mbele ya Msalaba ama pamoja na kielelezo cha Taswira ya Bikira Maria.

...Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu.Amina

...Sali sala ya Uje Roho Mtakatifu au wimbo wa Uje Roho Mtakatifu..

Sala ya uje Roho Mtakatifu.

Uje Roho Mtakatifu uzinee roho za waumini wako, washa ndani moto wa mapendo yako, peleka roho wako, vitaumbwa upya na nchi zitageuka.

Tuombe: Ee Mungu uliyependa kuzifurahisha nyoyo za waumini wako ukiwaletea mwanga wa Roho Mtakatifu, tunaomba tuongozwe na yule Roho, tupende yaliyo mema , tupate daima faraja zake. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristu bwana wetu. Amina.

2.SALA YA TOBA

Ee Mungu wangu ninakusadiki, ninakutumainia, ninakuabudu,na ninakupenda. Kwako ninawaombea msamaha wale wote wasiokusadiki, wasiokuabudu, wasiokutumainia na wasiokupenda.

3. SALA YA KUOMBA KIFO CHEMA.

Ee Bwana na mwokozi wangu, nisaidie katika saa hiyo katika mikono yenyeye nguvu ya Sakramenti zako na kwa harufu nzuri ya faraja zako.Ruhusu maneno ya maondoleo ya dhambi yatamkwe juu yangu, na ishara ya mafuta matakatifu initie muhuri, na Mwili wako mwenyewe uwe chakula changu na Damu yako inifunike, na Malaika wangu aninong'oneze neno la amani na watakatifu wako watukufu wanitazame kwa tabasamu; ili kwamba kwa njia yao wote na kupitia kwao wote, nipokee zawadi ya uvumilivu, na nife kama ninavyotamani kuishi, katika Imani yako, katika Kanisa lako, katika kukutumikia, na katika Upendo wako. Amina

4. SALA YA SIKU (*inabadilika kulingana na tarehe ya siku*)

5. SALA YA MWISHO

Ee Utatu Mtakatifu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, ninakuabudu kwa heshima kubwa sana. Nakutolea Mwili na Damu azizi, Roho na Umungu wa Yesu Kristo, vilivyomo katika Tabernakulo zote duniani, kwa malipizi ya dhambi zinazomtia uchungu. Na, kwa mastahili yasiyo na mipaka ya Moyo Mtakatifu wa Yesu, na kwa maombezi ya Moyo Safi wa Maria, naomba wakosefu maskini waongoke. Amina

Bikira Maria wa Fatima....Utuombee

Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina

SIKU YA KWANZA 04/05/2022 (JUMATANO)

Nia ya Pamoja;

Tunamshukuru Mungu kwa wagonjwa wa corona walioponywa na kukingwa na janga hili.

Tunakuomba Mama Yetu wa Fatima utuondolee gonjwa hili la Corona pamoja na magonjwa mengine yasiyo na tiba.

Ee Mama yetu wa Fatima, uliyetokea Fatima na kuwafunulia watoto wachungaji fadhila za neema zilizofichika za kusali rozari, kufanya malipizi, toba na sadaka, uifanye mioyo yetu ipende kusali rozari, kufanya toba, kufanya malipizi na kutolea sadaka ili kwa kutafakari mafumbo ya wokovu wetu, ambayo yamo katika rozari tupate matunda ya rozari, wongofu wa wakosefu, amani duniani na neema hii ninayoiomba kwa bidii.

Ee Mama Maria, mama yetu wa Fatima leo ninakuja mbele yako, nikiomba kwa maombezi yako ya kimama, njaliwe (.....hana taja ombi lako)

Baba Yetu x3 Salaam Maria x3 na Atukuzwe Baba x3

Sali mafungu matano ya Rozari Takatifu ya siku husika.

SIKU YA PILI 05/05/2022(ALHAMIS)

Nia ya Pamoja;

Tunayaombea mataifa yote yanayopigana vita ikiwemo Urusi na Yukrenia yaweze kutatua migogoro yao kwa njia ya amani ili watu wake wafurahie tunu ya zawadi ya maisha.

Ee Mama yetu wa Fatima, uliwatokea watoto wachungungaji katika Shimo la Amani “Cova da Iria” Ikiwa ni jibu la novena ya kumuomba Moyo Mtakatifu wa Yesu arejeshe amani duniani kwa njia ya Maria dhidi ya vita vya kwanza vya dunia.Ikiwa ni agizo la Baba Mt. Benedikto XV. Tunaomba mama ukomeshe vita, ulete amani duniani kwa njia ya sisi kusali Rozari Kila siku.

Ee Mama Maria, mama yetu wa Fatima leo ninakuja mbele yako, nikiomba kwa maombezi yako ya kimama, njaliwe (.....hana taja ombi lako)

Baba yetu x3, Salaam Maria x3 na Atukuzwe Baba x3

Sali Mafungu matano ya Rozari Takatifu ya siku husika

SIKU YA TATU 06/05/2022 (IJUMAA)

Nia ya Pamoja;

Tuwaombee Huruma ya Mungu wanaofanya kufuru zote katika sakramenti kuu ya Altare sambamba na wanabomoa makanisa na kuharibu matakatifu. Tuombe usalama wa Sakramenti kuu katika Tabernaklo sambamba na kuwaombea usalama Makasisi wetu.

Ee Mama Yetu Bikira Maria wa Fatima, kabla ya Matokeo yako, wachungaji watoto walitokewa na Malaika mara tatu kwa lengo la kuwandaan na kuwaimarisha. Katika matokeo hayo malaika aliwaalika watoto wachungaji kusali naye, kufanya majitoleo na kuwaimarisha kwa sakramenti ya Ekaristi Takatifu na aliwafundisha kutolea sadaka hiyo takatifu kwa ajili ya kulipia dhambi zinazomchukiza Mungu. Tunakuomba ewe mama yetu wa Fatima tujaliwe fadhila ya utii wa sauti ya Mungu na Malaika mlinzi, kufanya malipizi na kujitoa sadaka kwa ajili ya wengine katika kuishi kitakatifu na hasa maisha ya sala kwa kuwa Moyo Mtakatifu wa Yesu na Moyo wako Immakulata unasikiliza sala zetu.

Ee Mama yetu wa Fatima leo ninakuja mbele yako, nikiomba kwa maombezi yako ya kimama nijaliwe (.....hana taja ombi lako)

Baba yetu x3, Salaam Maria x3 na Atukuzwe Baba x3

Sali Mafungu matano ya Rozari Takatifu ya siku husika

SIKU YA NNE 07/05/2022 (JUMAMOSI)

Nia ya Pamoja;

Kuiombea amani nchi yetu ya Tanzania, hali ya uchumi wa nchi na raia wake pamoja na hali ya hewa hususani mvua ili tuepukane na njaa na ukame .

Ee Mama Yetu Bikira Maria wa Fatima; Malaika wa amani aliwasisitiza wachungaji watoto watatu kusali zaidi na wafanye chochote watakachowea kumtolea Mungu sadaka kwa ajili ya kulipia dhambi zinazomchukiza na kwa ajili ya wongofu wa wakosefu. Na kwa jinsi hii amani itapatikana duniani. Na zaidi sana Malaika wa amani huyo aliwasihii kuvumilia bila manung'uniko mateso yote ambayo Bwana atawaletaa.

Ee Mama yetu wa Fatima, tunaomba fadhila ya Unyenyekevu na uvumilivu tunapoonewa na kudharauliwa. Tuvumilie na kusali zaidi mpaka mwisho huku

tukiyatolea hayo sadaka na kufanya malipizi kwa ajili yetu na kwa ajili ya wengine. Mama Maria, tufanye tuwe vyombo vya amani duniani hapa.

Ee Mama yetu wa Fatima, leo ninakuja mbele yako nikiomba kwa maombezi yako ya kimama njialiwe (.....hana taja Ombi lako)

Baba yetu x3, Salaam Maria x3 na Atukuzwe Baba x3

Sali Mafungu matano ya Rozari Takatifu ya siku husika

SIKU YA TANO 08/05/2022 (JUMAPILI)

Nia ya Pamoja;

Tuziombee familia zetu ziweze kuchipusha na kustawisha maadili mema na kutunza uhai.

Ee mama yetu wa Fatima tunaona huzuni kubwa ya moyo wako wa kimama juu ya dhambi za dunia na makufuru yanayoendelea dhidi ya amri za Mungu na hivyo kuwatia watu katika hatari ya kutupwa kwenye ziwa la moto wa milele. Mama, unahuzunishwa kwa ajili ya watoto wako duniani.Tunaomba utujalie fadhila ya kuepuka nafasi za dhambi na visa vyenye kulturejesha dhambini.Tunaomba neema ya kuishi kitakatifu kama watoto wachungaji Lucia , Fransisko na Yasinta.Tunaomba toba kwa ajili yetu wenywewe na dunia nzima.Tunaahidi kufanya malipizi, sala na sadaka ili tusimkosee Mungu zaidi kwani tumemkosea sana mpaka sasa.

Ee Mama yetu wa Fatima, leo ninakuja mbele yako nikiomba kwa maombezi yako ya kimama njialiwe (.....hana taja Ombi lako)

Baba yetu x3, Salaam Maria x3 na Atukuzwe Baba x3

Sali Mafungu matano ya Rozari Takatifu ya siku husika

SIKU YA SITA 09/05/2022 (JUMATATU)

Nia ya Pamoja;

Kuomba neema ya kuipenda sala ya rozari na kusali rozari kwa uchajji

Ee Mama yetu wa Fatima katika matokeo yako ulisisitiza tusali Rozari na tutolee sadaka kwa ajili ya wakosefu wapate kuongoka.Mama, ulisema watu wengi wanakwenda motoni kwa sababu hakuna anayejishughilisha kuwaombea na kutolea sadaka kwa ajili

yao.Tunaomba utujalie neema ya kuipenda sana Ibada ya Rozari takatifu, iliyo ya pili kwa ukuu kutoka ile ya sakramenti kuu.Tujalie mama Neema ya Kusali rozari kwa uchaji na tafakari, tukiyatafakari mafumbo ya ukombozi wetu kwa njia ya Maria.

Ee Mama yetu wa Fatima, leo ninakuja mbele yako nikiomba kwa maombezi yako ya kimama njialiwe (.....hana taja Ombi lako)

Baba yetu x3, Salaam Maria x3 na Atukuzwe Baba x3

Sali Mafungu matano ya Rozari Takatifu ya siku husika

SIKU YA SABA 10/05/2022 (JUMANNE)

Nia ya Pamoja;

Tuwaombee wagonjwa wote wapate neema ya uvumilivu na ustahimilivu na watakaokufa wafe kifo chema mikononi mwa Yesu na Maria.

Ee Mama yetu wa Fatima katika tokeo lako la pili na la tatu kule Fatima Bwana alianzisha ibada kwa Moyo wako safi usio na doa na kuahidi ya kwamba watu watakaoizingatia Ibada hiyo wataokoka kwa kuwa utawajalia neema ya wokovu ile saa ya kufa. Tunakuomba mama utuwezeshe kupokea kwa hiari mikononi mwako kifo tulichopangiwa. Tunaomba fadhila na mastahili ya kuiheshimu jumamosi ya kwanza ya kila mwezi katika mazingira yetu kwa ajili ya kufanya toba, kufanya malipizi, kusali rozari takatifu kwa nia ya kuwaombea wakosefu waongoke , kutafakari maisha ya Yesu na Maria na kupokea komnio ya malipizi ili kuufariji moyo wako safi usio na doa dhidi ya machukizo na ukosefu wa shukrani. Ee Maria Immaculata, tunaomba mama kupata tunza yako ya kimama ndani ya moyo wako safi usio na doa ili roho nydingi ziokolewe na ili tupate amani duniani, familia zetu zipate hifadhi ndani ya Moyo wako safi usio na doa .

Ee Mama yetu wa Fatima, leo ninakuja mbele yako nikiomba kwa maombezi yako ya kimama njialiwe (.....hana taja Ombi lako)

Baba yetu x3, Salaam Maria x3 na Atukuzwe Baba x3

Sali Mafungu matano ya Rozari Takatifu ya siku husika

SIKU YA NANE 11/05/2022 (JUMATANO)

Nia ya Pamoja;

Tuwaombee watu wenyе mahitaji maalumu, walioko pembezoni, waliotengwa, wanaoteswa na kukosewa haki .Mungu awape faraja na matumaini.

Ee Mama Yetu wa Fatima, uliwaonyesha njozi ya moto wa milele Lucia , Fransisko na Yasinta.Njozi iliyowatisha hata walitetemeka kwa hofu.

Hapa mama ulisema ukijaa wema na uchungu mkubwa: “wakosefu wako njiani mwa kuuendea”. Kusudi waokolewe Bwana alianzisha ibada kwa moyo wako safi.

Tunakuomba mama yetu wa Fatima bondeni huku kwenye machozi, usituache tukatelezea majoribuni na katika maelekeo ya dhambi.Ee mama yetu utuepushe na moto wa milele ndani ya tunza yako ya kimama ndani ya moyo wako safi usio na doa.Tusaidie tusali zaidi rozari yako ili roho nyingi ziokoke na moto huo wa milele, tutoe sadaka, majitoleo na malipizi kwa ajili yao.Tuige mfano wa maisha ya sala ya Lucia Fransisko na Yasinta.

Ee Mama yetu wa Fatima, leo ninakuja mbele yako nikiomba kwa maombezi yako ya kimama nijaliwe (.....hana taja Ombi lako)

Baba yetu x3, Salaam Maria x3 na Atukuzwe Baba x3

Sali Mafungu matano ya Rozari Takatifu ya siku husika

SIKU YA TISA 12/05/2022 (ALHAMIS)

Nia ya Pamoja;

Tuziombee familia zetu ziwe na umoja , maelewano, upendo, usawa,mshikamano na Huruma. Wanafamilia waishi kwa kusameheana na kuchukuliana kwa kuwa Mungu ni upendo na anaishi ndani mwetu.

Ee mama yetu wa Fatima katika tokeo lako la tano mwezi septemba uliwaahidi watoto kurudi mwezi Oktoba pamoja na Mtakatifu Yosefu na Mtoto Yesu. Na kweli mama ukiwa mwenye huzuni kubwa ultokea na kumwambia Lucia kanisa lijengwe mahali pale kwa heshima yako, watu waendelee kusali rozari na wasiendelee kumkosea bwana Mungu wetu zaidi ya wanavyofanya sasa;kwani ameshachukizwa kiasi cha kutosha.

Ujumbe huu ulikuwa ni wa dunia nzima hata leo.Ee Mtakatifu Yosefu uliyetumwa na Mama Bikira Maria pale Fatima kuibariki dunia na kuiletea amani, tupatie na sisi uimara wako katika neema, utii wako kwa maisha ya kiroho , upendo wako kwa Maria na upendo wako kwa mtoto Yesu.

Ee familia takatifu ya Nazareti, tusaidieni tunapokabiliwa na changamoto za kifamilia. Tunaomba msaada wenu katika sala, familia zisali rozari pamoja. Tusaidieni kutovunjika moyo hata wakati magumu na shida mbalimbali za maisha zinapoelekea kutuvunja moyo. Ee mama yetu wa Fatima, ongeza Imani yetu; tushauri tuwapo na mashaka, tushike mkono tuwapo dhaifu, na tutulize katika huzuni. Kwako mama wa Fatima tunaziaminisha familia zetu, wazazi, watoto, ndugu, wagonjwa waliomo, na familia zote zinazoteseka.Ziombee familia zote ziwe na amani, maelewano na mapendo ya kweli kati yao. Wasaidie wanafamilia kuishi kwa upendo, kusameheana na kuishi kwa njia ya amani katika yote wakizishika amri za Mungu.

Ee Mama yetu wa Fatima, leo ninakuja mbele yako nikiomba kwa maombezi yako ya kimama nijaliwe (.....hapa taja Ombi lako)

Baba yetu x3, Salaam Maria x3 na Atukuzwe Baba x3

Sali Mafungu matano ya Rozari Takatifu ya siku husika

Novena Hii imetungwa na Fortunata de Maria Masaka

Mratibu Rozari Hai.

0717558222

Parokia ya Mt.Rita wa kashia Goba.

Dar es salaam

******AVE MARIA !!!!**** (“Salini Rozari”-Bikira Maria Fatima 1917)**

MAPENDO NI YA MILELE